



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. MDC/CL.20/5/VOL. I/10

21/12/2021

MKURUGENZI MTENDAJI,
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA,
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

Kuh. KUTHIBITISHA UMILIKI WA ARDHI ENEO LA TAWETA

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

2. Ofisi yangu inakiri kupokea barua kutoka Kampuni ya Tova Land Company Limited wa S.L.P 80072, Dar es salaam kuhusu mada tajwa hapo juu ikiwa na dhamira ya kutaka atambulike rasmi kuwa mwekezaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba Kata ya Masagati Kijiji cha Taweta. Aidha, kutokana na uhakiki uliofanywa kupitia kikao cha Halmashauri ya Kijiji cha Taweta, Mkutano mkuu wa Kijiji pamoja na kutembelea eneo analotaka kuwekeza, wananchi walifafanua kuwa Ardhi hiyo imenunuliwa kutoka kwa watu. Taratibu za kampuni ya TOVA kujadiliwa kwenye kikao cha Halmashauri ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa Kijiji zimekamiliwa.
3. Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 inaweka utaratibu wa utwaji Ardhi ya Kijiji ambapo ni sharti mwombaji ajadiliwe kwenye kikao cha Halmashauri ya Kijiji pamoja na Mkutano Mkuu. Pia mwombaji wa Ardhi ni sharti ajadiliwe kwenye kamati ya ugawaji Ardhi ya Wilaya kwa Ardhi inayoanzia ekari 50 hadi 500 na Kamati ya Kitaifa kwa Ardhi yenye ukubwa wa ekari zaidi ya 500.
4. Kwa barua hii napenda kuitambulisha Kampuni ya Tova kama mmiliki wa Ardhi yenye ukubwa wa ekari 2628 katika Kijiji cha Taweta. Aidha, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya inatambua dhamira ya Kampuni hiyo kuhusu kuwekeza katika Ardhi ya Kijiji cha Taweta kutokana na eneo ambalo imenunua kutoka kwa wananchi, Kampuni hiyo inawajibika kutimiza takwa la sheria ndogo za Halmashauri ya Wilaya ambapo italazimika kulipa gharama za huduma za Ardhi kiasi cha shilingi 10,000.00 kwa kila ekari ili taratibu zingine za umilikishaji ziweze kuendelea kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

Nakutakia utekelezaji mwema


Wakili Nakua F.A,
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (WA)
MLIMBA. For: DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
MLIMBA